

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO**

**SHULE YA SEKONDARI NGWELO**

**S. L. P 368**

**LUSHOTO.**

**...../12/20.....**

Kumb. Na. NSS/JJ/2020

JINA LA MWANAFUNZI \_\_\_\_\_

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI  
NGWELO MWAKA 2021.**

**1.0 UTANGULIZI**

Uongozi wa shule ya sekondari ngwelo, unayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kuingia kidato cha kwanza katika shule ya sekondari ngwelo. Unapongezwa sana kwa kuwa mionganini mwa vijana wachache waliochaguliwa(waliopata nafasi ya kujiunga na shule za sekondari za serikali.

Tunategemea utalienzi taifa lako kwa kufanya bidii katika masomo na kila shughuli shulenii na kutumia nafasi hii vizuri.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 04/01/2021. Unatakiwa kuripoti shulenii tarehe 04/01/2021 na mwisho wa kulipoti ni tarehe 15/01/2021 ndani ya siku kumi za masomo.

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1 SARE YA SHULE**

a) **WAVULANA**

- MASHATI MEUPE YA MIKONO MIFUPI YASIYOBANA(Unashauriwa yawe ya tomato)
- Suruali mbili rangi ya kijivu zenyne marinda mawili zisizo bana
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kisigino kifupi vya kufunga na kamba (jozi mbili)
- Soksi ndefu nyeusi jozi zisizopungua mbili
- Sweta la rangi ya kijivu lenye shingo ya “V” na tai ya rangi yakijivu

b) WASICHANA

- Mashati mawili meupe ya mikono mifupi yasiyobana ( unashauriwa yawe ya tomato)
- Sketi ndefu chini ya magoti rangi ya kijivu zenyenye marinda nane
- Kwa waislamu wanaruhusiwa kuvaahijabu nyeupe inayofika kwenye kifundo cha mikono pamoja na nusu kanzu.
- Viatu vyeusi nya ngozi vyenye kisigino kifupi nya kufunga kwa kamba.
- Soksi ndefu nyeupe .
- Sweta la rangi ya kijivu lenye shingo ya “ V ” na tai ya rangi ya kijivu.

(c) Kila mwanafunzi awe na nguo za michezo ambazo ni t-shirt nyekundu isiyo na maandishi, trak suit nyeusi yenyenye mistari myeupe ( kwa wavulana ) na track suit ya rangi ya bluu yenyenye mistari myeupe ( kwa wasichana ) pamoja na bukta na raba.

## 2.2 VIFAA MUHIMU KWA MATUMIZI YA KILA SIKU

Mwanafunzi anatakiwa awe na daftari kubwa kumi ( quire 3), Daftari nyingine ndogo kwa ajili ya mazoezi ya kila somo, seti ya vifaa nya hisabati, kalamu za wino za kutosha, penseli, kifutio, rula ndefu na dictionary moja.

NB: vifaa hivi vitakaguliwa siku ya kuripoti.

## 2.3 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.

Sheria na kanuni hizi ni za muhimu na zieleweke kuwa ndio dira na usalama wako shuleni.

(a) SHERIA ZA NCHI

Kila mwanafunzi analazimika kufuata sheria zote za nchi. Ni wajibu kuheshimu Bendera ya Taifa, picha za viongozi wa Taifa, Wimbo wa Taifa, Fedha ya Taifa na Nembo ya Taifa.

(b) MASOMO

Shughuli zote zilizopangwa katika ratiba ya shule ni muhimu. Kila mwanafunzi anatakiwa kufuata ratiba ya shule kama ilivyopangwa. Mwanafunzi anatakiwa kuwahi shuleni asubuhi na abaki shuleni hadi mwisho wa shughuli za siku. Mwanafunzi ataondoka shuleni kwa ruhusa maalumu ( Pass ) tu.

(c) MAADILI

i. HESHIMA

Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu walimu, Wafanyakazi wa shule, Viranja, Wananchi na wanafunzi wenzake hapa shuleni na nje ya shule.

ii. USAFI

Usafi wa mwili na mavazi ni muhimu hapa shulenii

iii. NI MWIKO KWA MWANAFUNZI

Kuvuta sigara, bangi, kutumia madawa ya kulevyaa na kunywa pombe.

Kutembelea vilabu nya pombe, majumba ya starehe au majumba ya kufikia wageni.

Kutumia lugha mbaya na za kihuni kwa wanafunzi wenzako, kwa walimu na kwa watu wengine.

iv. NI MARUFUKU KWA MWAFUNZI

Kujipamba, kutia dawa nywele, kupaka kucha rangi, kupaka midomo rangi, kuvaan bangili, kuvaan mikanda mipana, kuandika maandishi kwenye mwili au mavazi.

Hairuhusiwi kunyoa mitindo ya kihuni, kuvaan kofia, kuvaan viatu nya ghorofa na mikufu ya shingoni.

**V. UVAAJI WA SARE NI LAZIMA KWA WANAFUNZI WOTE WAKATI WA**

- Masomo darasani
- Wanafunzi wanapotoka nje ya shule kwa shughuli za kishule
- Maandamano
- Wanafunzi wanapokwenda hospitali
- Mikutano
- Mhadhara wa shule (school Baraza)

**VI.TUNZA MAJENGO,SAMANI, VITABU NA VIFAA VYOTE VYA SHULE VIZURI**

Asiyetunza vifaa na kutumia vizuri mali ya shule ataadhidiwa vikali na kufidia gharama ya uharibifu.

d) MIKUTANO NA MAWASILIANO

Mikutano na mawasiliano ya aina yoyote hapa shulenii lazima ijulikane rasmi kwa Mkuu wa shule

e) LUGHA

Masomo yote isipokuwa somo la kiswahili na Elimu ya Dini ya Kiislamu yanafundishwa kwa Kiswahili.

Tunasisitiza Kiingereza kuwa lugha rasmi shulenii. Kila mwanafunzi ajitahidi kukuza ufaahamu wake katika kuongea na kuandika kiingereza.

## **2.4 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE**

- i. Wizi
- ii. Uasherati na ushoga
- iii. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyta, kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k
- iv. Kupiga au kupigana
- v. Kuharibu kwa maksudi mali ya umma
- vi. Kudharau bendera ya taifa
- vii. Kuwa mjamzito au kupata mimba
- viii. Kuoa au kuolewa
- ix. Kutoa mimba
- x. Kugoma, kuchochea au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- xi. Kukataa adhabu kwa makusudi.
- xii. Kuwa na simu ya mkononi.

## **3.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.**

- A. Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara watakapo ripoti shulenii.
- B. Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
- C. Fomu ya mzazi/mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

## **4.0 TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEKEZO/ MAAGIZO NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

.....

**MZEE R. SUDI**

**MKUU WA SHULE**

**GOVERNMENT OF  
TANZANIA  
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

SHULE YA SEKONDARI NGWELO

S. L. P 368

LUSHOTO.

...../12/20.....

MEDICAL OFFICER,

\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_

MR/ \_\_\_\_\_

Please examine the above named pupil that he/she is physical and mental fit/unfit for full time schooling course

(a) (i) eye sight\_\_\_\_\_

(ii) Limbs\_\_\_\_\_

(iii) Speech\_\_\_\_\_

(v) Venereal disease\_\_\_\_\_

(vi) Leprosy\_\_\_\_\_

(vii) Epilepsy \_\_\_\_\_

(b) Neuroses\_\_\_\_\_

(c) Other serious disease (**mention**)  
\_\_\_\_\_

Pregnant test\_\_\_\_\_

Other important test (**if  
any**)\_\_\_\_\_

Station\_\_\_\_\_ Name\_\_\_\_\_ Sign  
ature\_\_\_\_\_

Designation\_\_\_\_\_